TAARIFA FUPI YA KITAALAM YA UFUNGUZI WA MRADI WA VITUO VYA UOKOZI NA UZAMIAJI ZANZIBAR - MKOANI PEMBA IKIWASILISHWA NA KATIBU MKUU OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

- Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dr. Ali Mohammed Shein.
- Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.
- Waheshimiwa Mawaziri mliopo.
- Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa Kusini Pemba
- Waheshimiwa viongozi mbali mbali wa chama na Serikali mliopo
- Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama mliopo
- Maafisa na wapiganaji wa KMKM.
- Ndugu wananchi

ASSALAM ALAYKUM

Mheshimiwa mgeni Rasmi

Kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutukutanisha hapa tukiwa wazima wa afya katika siku hii muhimu na adhimu ya uzinduzi wa vituo vya Uokozi na Uzamiaji Zanzibar.

Aidha kwa niaba ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ninapenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Mgeni rasmi, kwa kujumuika nasi katika shamra shamra hizi za kuadhimisha miaka 55 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Mheshimiwa Rais,

Mradi huu wa ujenzi wa Vituo vya Uokozi na Uzamiaji Zanzibar ni wa miaka minne na ulianza

rasmi mwaka wa fedha 2014/15 na ulipangiwa kutumia Tzs. 5,916,842,500/-hadi kukamilika kwake. Hata hivyo gharama hizi ziliongezeka kulingana na mabadiliko ya thamani ya vifaa vilivyokadiriwa kununuliwa.

Mradi huu wa vituo vya Uzamiaji na Uokozi ni utekelezaji kwa vitendo wa malengo halisi ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964 na vile vile ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2015/2020 katika kuimarisha ulinzi na usalama wa maisha ya wananchi pamoja na kuzijengea uwezo vikosi Idara Maalum za SMZ.

Mheshimiwa Rais,

Mradi huu una maeneo makuu manne ambayo ni:

1. Ujenzi wa vituo vya Uokozi na Uzamiaji
2. Ununuzi wa boti za uokozi na vifaa vya uzamiaji
3. Ununuzi wa vifaa vya mawasiliano na

4. Kuwapatia mafunzo maofisa na wapiganaji pamoja na wananchi.

Mradi ulikusudia kujenga vituo sita (6) vya uokozi na uzamiaji lakini umekamilisha vituo vitatu ambavyo ni Kibweni na Nungwi (kwa Unguja) na Mkoani (kwa Pemba). Na vituo vitatu ambavyo ni Kizimkazi, Wete na Msuka vitajengwa sambamba na ujenzi wa mahanga ya askari kuanzia mwaka wa fedha 2019/2020. Vituo vilivyokamilika vimegharimu Shilingi 966,842,550/=

Mheshimiwa Rais,

Mradi ulilenga kununua boti mbili za uokozi ambazo tayari zimeshanunuliwa. Boti hizi zina uwezo wa kukimbia *Knotical mile 55* kwa saa ambazo ni sawa na Kilomita 99, na zina vifaa maalum vyenye uwezo wa kuokoa hadi watu 400 kwa boti ndogo na watu 600 kwa boti kubwa kwa wakati mmoja. Aidha boti ndogo ina uwezo wa kubeba hadi watu 20 na boti kubwa watu 40 na kuwakimbiza katika kituo kwa

kupata huduma. Boti hizi zimegharimu jumla ya Shilingi 12,500,000,000/-

Kwa upande wa vifaa vya uzamiaji vilivyonunuliwa ni pamoja na nguo maalum za uzamiaji, mitungi ya gesi, mashine ya kutengenezea gesi na vifaa mbalimbali vya kutumia chini ya bahari wakati wa uokozi. Vifaa hivi vimegharimu Shilingi 500,000,000/-

Aidha vifaa vya mawasiliano vimejumuisha Mtambo wa Redio (Radio Base), Rada ya Baharini (Marine Radar), Kompyuta na vifaa vya GPS ambavyo vimegharimu Shilingi 470,000,000/-

Mheshimiwa Rais,

Kupitia Mradi huu, Maofisa na wapiganaji 68 wa KMKM wamepatiwa mafunzo ya namna ya kutumia vifaa vilivyomo katika mradi huu. Pia wananchi 850 wanaofanya shughuli za uvuvi na wasafirishaji wadogo wadogo wa abiria na mizigo katika Mikoa Mitano ya Zanzibar wamejengewa uelewa wa kuwepo kwa Mradi huu na wamepatiwa mafunzo ya kutumia

vifaa vya mawasiliano kwa ajili ya kutoa taarifa wanapohitaji msaada wakiwa baharini. Miongoni mwao wameanza kuvitumia vituo hivyo wanapohitaji msaada. Mafunzo hayo yamegharimu Shilingi 30,000,000/=

Mheshimiwa Rais,

Mbali ya vifaa vilivyopatikana kupitia Mradi huu, Ofisi imepanga kuvipatia vituo hivi DRONE moja kati ya tatu zilizonunuliwa kupitia Mradi wa Mji Salama ili kuimarisha ulinzi wa baharini kwa njia ya anga. Aidha Kikosi cha KMKM kimenunua kifaa maalum (Decompression Chamber) ambacho kitatumika kuwasaidia wahanga walioathirika katika mfumo wa kupumua kupata huduma ya kwanza na kuweza kurejea katika hali ya kawaida.

Kukamilika kwa mradi huu kutaleta mapinduzi makubwa katika sekta ya usafiri wa baharini kwa kuimarisha usalama wa wananchi hususan wale wanaotumia bahari katika shughuli zao za kila siku.

Mheshimiwa Rais,

Maofisa na Wapiganaji wa KMKM wanakuahidi kuvilinda na kuvitunza pamoja na kuvitumia vizuri vifaa vya Uokozi ili kuweza kuifanya huduma ya usafiri baharini kuwa katika hali ya usalama mkubwa.

Mwisho kabisa naomba nitumie fursa hii kumkaribisha Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ azungumze machache na kisha akukukaribishe Mheshimiwa Mgeni Rasmi, ili uzungumze na hadhara hii iliopo mbele yako katika uzinduzi wa vituo vya uokozi na uzamiaji.

Karibu Mheshimiwa.

MAPINDUZIIIIIIIII